HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, naanza kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako kwanza kwa kumshukuru Mwenyezimungu Mtukufu kwa kutuamsha hai na afya njema siku ya leo tukiwa ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Tunamuomba Mwenyezimungu kwa baraka za mwezi huu atakabali ibada zetu na ajaliye tuteleze majukumu yetu haya ya kuwatumikia wananchi kwa salama mpaka tuhitimishe.

Mheshimiwa Spika, nakushuru wewe kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kusimama hapa kwa niaba ya Mwenyekiti kuwasilisha maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2018/19.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa naomba kuchukuwa fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa juhudi kubwa anazochukuwa za kuimarisha miundombinu ya elimu na hatua madhubuti za kuhakikisha kuwa vijana wetu wanapata elimu bure kuanzia elimu ya Maandalizi mpaka sekondari.

Mheshimiwa Spika, Ni hivi juzi tu Mheshimiwa Rais amezindua mpango wa ruzuku kwa Skuli, Jambo hili ni kubwa na hatuna budi kwa dhati kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuacha alama kubwa ya uongozi katika sekta ya elimu Zanzibar, ikiwa pia ni kudumisha sera ya elimu bila malipo iliyoasisiwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar Mzee Abeid Amani Karume na chama cha Afro-Shirazi ambayo ni matunda ya Mapinduzi yetu matukufu ya mwaka 1964.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kumshukuru Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mheshimiwa Riziki Pembe Juma ambaye muda mfupi uliopita amewasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yake kwa weledi na ufasaha mkubwa, aidha nimshkuru pia Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mheshimiwa Mmanga Mjengo Mjawiri na watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Idriss Muslih Hija, Naibu Katibu Mkuu Taaluma Bi. Madina Mjaka Mwinyi, Naibu Katibu Mkuu Utawala Maalim Abdalla, Wakurugenzi wote wa Wizara, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na watendaji wake, Wakuu wa Taasisi za Wizara, Vitengo, Maafisi mbali mbali waandamizi wa Wizara, Walimu Wakuu wa skuli zote za Unguja na Pemba, ndugu zetu walimu wa kada zote kuanzia maandalizi, Msingi, sekondari, vyuo an vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inawapongeza viongozi wote hawa kwanza kwa kazi kubwa wanazofanya kuhakikisha kuwa sekta ya elimu inaendelea pamoja na changamoto kadhaa zinazowakabili. Lakini pia kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia

Kamati ya Ustawi wa Jamii wakati wote ikifanya majukumu ya kusimamia utekelezaji wa kazi na majukumu yake katika kipindi chote cha miaka miwili ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, Naomba nikiri kuwa kutokana na mashirikiano hayo katika kipindi chote hicho, Kamati yangu tumejifunza na kufahamu mambo mengi yanayohusu sekta hii ya elimu, aidha Kamati imeona mafanikio mengi yaliyopatikana katika sekta ya Elimu ambayo yametokana na juhudi kubwa za Serikali na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein. Lazima nikiri kuwa juhudi za Mheshimiwa Rais za kuimarisha miundombinu ya elimu katika kipindi kifupi zimesaidia sana kuimarisha elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kamati yangu pamoja na changamoto kadhaa zilizojitokeza wakati wa kufanya kazi za Kamati kama vile ufinyu wa mda na wingi wa majukumu, imefanyakazi kwa mashirikiano makubwa na Wajumbe wote wa Kamati ambao kutokana na ujasiri na umadhubuti wao wa kuhoja na kusimamia kazi za kamati wameniwezesha leo kusimama hapa na kuwasilisha hotuba hii kwa niaba yao. Naomba nitambuwe mchango wao mkubwa na wa thamani kwa kuwataja majina yao kama ifuataavyo:-

1. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame — Mwenyekiti
2. Mhe. Tatu Mohammed Ussi — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma — Mjumbe

4. Mhe. Viwe Khamis Abdalla Mjumbe

5. Mhe. Makame Said Juma Mjumbe

6. Mhe. Masoud Abrahman Masoud Mjumbe

7. Mhe. Hidaya Ali Makame Mjumbe

8. Ndg. Aziza Wazir Kheir Katibu

9. Ndg. Khamis Hamadi Haji Katibu

Mheshimiwa Spika, naomba niwe mwingi wa shukurani kwa kukushukuru wewe kwa kutuongoza vyema na kutushauri katika kazi zetu za Kamati, aidha nimshukuru kwa dhati Katibu wa Baraza ndugu Raya Issa Msellem na watendaji wake. Pamoja na mratibu wetu wa kazi za Kamati za Baraza la Wawakilishi ndugu Ramadhan Khamis Masoud kwa kweli wamefanya kazi kubwa kuhakikisha kuwa Kamati yetu inapata matayarisho ya kutosha ya kuwezesha kufanyakazi zake kwa ufanisi. Nawashukuru sana.

2. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ustawi wa Jamii imepitia fungu K01 la Wizara ya Elimu na Mafunzo Amali na baada ya mashauriano mbali mbali Kamati imelipitisha fungu hilo kwa ajili ya kuwasilishwa katika Baraza lako hili kwa ajili ya kujadiliwa na Wajumbe wote na hatimaye kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imepitia programu kuu na programu ndogo zilizomo katika fungu hili la Wizara na kwa ujumla Kamati inatoa maoni yafuatayo kwa kila programu kama ifuatavyo:-

1. PROGRAMU YA ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

Mheshimiwa Spika, programu hii muhimu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndiyo msingi wa elimu ya vijana wetu na ndipo wanapoanza kupikwa kuelekea katika hatua za juu za elimu na mustakbali wao. Kamati ya Ustawi wa Jamii imepitia fungu la programu hii pamoja na utekelezaji wake wa kazi mbali mbali katika bajeti inayomalizika ya 2017/18 na kwa ujumla imeridhika kiasi cha fedha kilichopatikana hadi mwezi Machi mwaka 2018 ni asilimia 58 ya fedha za wafadhili na asilimia 71 ya fedha za SMZ.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua mabadiliko ya msingi ya uendeshaji wa programu hii ambayo mwaka wa fedha 2017/18 imetengewa shilingi bilioni 70.7 na katika bajeti ya mwaka huu kimetengwa kiasi cha shilingi bilioni 10.8 ambapo shilingi bilioni 55.2 zimetengwa kwa shughuli za ugatuzi wa Elimu ya Maandalizi na Msingi kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kugatuliwa kwa baadhi ya shughuli za elimu ya msingi kutoka katika programu hii na kupelekwa Serikali za Mitaa lakini bado zipo shughuli nyingi zimebakia ambazo Kamati itazitolea maoni yake. Katika programu hii Kamati yangu inapenda kuendelea kushauri mpango wa kutayarisha vijana

katika elimu ya maandalizi uimarishwe kwa kuweka miundombinu ya watoto kusomea kama vile madarasa na walimu wa kutosha. Vile vile Kamati inashauri wananchi waelimishwe vyema umuhimu wa kupeleka watoto katika skuli za maandalizi. Hii ndio kutekeleza sera ya Taifa ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatambua kuwa idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa inaongezeka kila mwaka na yapo baadhi ya maeneo yanakumbwa na uhaba wa madarasa na wingi wa wanafunzi hali ambayo inasababisha mazingira yasiyo rafiki ya kusomea vijana wetu. Hivyo bado tunashauri kuimarishwa Miundombinu ya madarasa na upatikanaji wa walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika programu hii Wizara pia inasimamia madarasa na vyuo vya Qur-an na wanamashirikiano makubwa na Ofisi ya Mufti. Kamati inashauri kuwa eneo hili liongezwe nguvu ya usimamizi hasa katika kuandaa mpango wa kusajili madarasa na vyuo vya Qur-an pamoja na kuweka mpango wa kusajili na kutoa leseni za walimu wanaosimamia vyuo na madara hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza utaratibu huo uendelee kwa nguvu kubwa kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na tatizo la usalama wa vijana wetu katika baadhi ya madarasa na vyuo vya Qur-an kutokana na kukithiri vitendo vya udhalilishaji. Baadhi ya wahalifu wa watoto wanajipenyeza katika madarasa na vyuo vya Qur-an kujifanya ama walimu au wasimamizi wa watoto na kuwafanyia vitendo viovu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inashauri kupitia programu hii na kwa kushirikiana na Ofisi ya Muft, kuandaa mpango wa kusajili vyuo na kuweka vigezo vya walimu hao kupata leseni ikiwemo uwekaji wa kumbukumbu za kiusalama za walimu wote wanaosajiliwa kusimamia vyuo na madrasa ikiwa pamoja na kujuwa taarifa mbali mbali za kihalifu za muhusika.

2. PROGRAMU YA ELIMU YA SEKONDARI

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu hii kifedha kwa mwaka wa bajeti unaomalizika umechangiwa sana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kiasi cha asilimia 68 cha Makadirio hadi kufikia mwezi Machi 2018. Hata hivyo kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kazi mbali mbali zimefanyika katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/18 na Kamati yangu imepita kuangalia utekelezaji wa kazi hizo katika maeneo mbali mbali. Kwa mwaka bajeti 2017/18 programu hii imetengewa shilingi bilioni 63.4 hata hivyo Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha hizo katika bajeti ya mwaka huu kufikia shilingi bilioni 95.5. tunashauri sana fedha hizo zopatikane katika utekelezaji wa programu hii.

Mheshimiwa Spika, Katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za programu hii Kamati yangu imefanya ziara ya kupitia Wilaya zote za Unguja na kukutana na walimu Wakuu na wanafunzi wa Skuli za Sekondari kwa madhumuni ya kujuwa changamoto mbali mbali zinazowakabili katika masomo yao husasan changamoto zinazosababisha kutofanya vizuri katika mitihani yao ya kitaifa.

Kamati imebaini mambo mengi sana ambayo yanakabili walimu, wanafunzi na maeneo ya kusomea. Baadhi ya mambo ambayo Wanafunzi hao wa Wilaya za Unguja na Walimu Wakuu wameyaeleza mbele ya Kamati na ambayo yanakwaza utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo:-

- Kamati imebaini Ubovu wa Miundombinu ya Skuli na uhaba wa huduma za jamii kama vile vyoo; zipo baadhi ya Skuli wanafunzi wamelalamika uhaba na ubovu wa madarasa na ukosefu wa vyoo vya kutosha.

- Kamati imebini pia Ukosefu wa vyumba vya maabara na vifaa; zipo Skuli kadhaa katika Wilaya hizo ambazo wanafunzi wanasomeshwa masomo ya Sayansi bila kuwepo maabara na vifaa vya maabara, sambamba na hilo zipo baadhi ambazo hazina walimu wa masomo hayo au zinakabiliwa na uchache wa walimu wa masomo ya sayansi.

- Uhaba wa vitabu vya kusomea na vikalio;

- Ukosefu wa mazingira tulivu ya kusomea kama vile dakhalia; wanafunzi wengi wameiambia kamati kuwa wanakosa utulivu wa kujiandaa na mitihani kwa kuwa wanalazimika kuwepo nje ya mazingira ya Skuli na kukumbana na changamoto za kijamii zinazorudisha nyuma maendeleo yao hasa wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wanafunzi kueleza hayo kwa kifupi, Kamati imebaini kuwa vijana wetu wengi hasa wa ngazi ya Sekondari hawashiriki kikamilifu katika masomo yao, wanafunzi wametuambia wenyewe kuwa wapo wanaojiingiza katika mapenzi, shughuli za kiuchumi kama vile utalii, matumizi ya simu na mitandao ya kijamii, kupoteza muda wa kuangalia filamu zenye makala ndefu (series) na utoro uliopindukia. Haya yote Kamati yangu imeyabaini kutoka kwa wanafunzi wenyewe na kwa kweli yanarudisha nyuma maendeleo ya elimu ya vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatoa wito kwa wazee kushirikiana na Walimu kuhusu maendeleo ya vijana wao, wasingoje mpaka matokeo ya mtihani yanatoka na kulalamika pale wanapobaini vijana wao wamefeli. Aidha Kamati za Skuli ziimarishwe na kuhakikisha vijana wanafuatiliwa nyendo zao wakiwa skuli na nyumbani na Kamati yangu inashauri sana Kamati za Skuli zipewe nguvu kwa kushirikiana na Serikali za mitaa hasa katika kufuatilia nyendo mbaya za vijana wetu. Lakini pia, tunatoa wito kwa vijana wetu hasa wa Sekondari kujitambuwa na kuachana na vitendo hivyo vinavyorejesha nyuma mustakabali wao wa baadaye.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na dhana ya muda mrefu kwa vijana wetu kuwa masomo ya Sayansi ni magumu na hivi sasa kumekuwa na kisingizio kuwa kuna uhaba wa walimu wa Sayansi na vifaa, ingawa hili ni kweli na Kamati imeona yenyewe, lakini bado Kamati inashangazwa na matokeo mabaya ya wanafuzi hata

kwa masomo ya sanaa ambayo yana walimu wa kutosha. Kamati yangu imetambuwa kuwa pamoja na kuwepo changamoto hizo bado sehemu kubwa ya mafanikio katika mitihani yapo kwa mwanafunzi mwenyewe kujibidiisha.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa programu ya elimu ya Sekondari kamati ilipata muda wa kuzungumza na walimu wakuu wa skuli za Wilaya za Unguja na kubaini kuwa zipo changamoto kadhaa zinawakabili katika utekelezaji wa majukmu yao kwa ujumla. Miongoni mwa changamoto hizo ni malimbikizo ya stahiki za walimu kama vile posho za likizo, masawazisho ya stahiki baada ya kumaliza masomo ya juu mishahara na posho za nauli.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa madeni haya yanawasononesha sana walimu, yanawatia unyonge walimu ambao wanapanda na kushuka Wizarani kufuatilia stahiki hizi. Kamati yangu kila ikipata fursa ya kukutana na walimu wanaonesha masikitiko hayo. Hivyo basi, kamati yangu imeshawasilisha kilio hichi cha walimu Wizarani na inakisema tena hapa ili Wizara na Serikali isikie na kuchukuwa hatua za kusawazisha malimbikizo hayo. Aidha Kamati hii inachukuwa ahadi kwa Walimu wote kuwa itafuatilia na kuhakikisha kuwa malimbikizo yao haya yanalipwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Kamati imepiga kelele kuhusu malipo ya nauli kwa walimu wanaoishi mbali na maeneo wanayosomesha. Viwango vya nauli vinavyolipwa ni vidogo na havina uhalisia wa malipo ya nauli zilivyo. Kamati imeambiwa

kuwa tatizo hili linasababishwa na kutotolewa viwango vipya vya nauli na Idara ya Usafirishaji na Leseni. Kamati imeshatoa ushauri ambao bado haujafanyiwa kazi kuwa Wizara ya Elimu ifanye Mawasiliano na Wizara inayohusika na Usafirishaji kupitia upya viwango vya nauli ili walimu walipwe nauli zinazolingana na maeneo wanayokwenda.

Mheshimiwa Spika, aidha kamati imeshauri pia Wizara ifikirie mpango wa kuanzisha usafiri wa kudumu wa kuwachukuwa walimu katika vituo vyao, mpango huu unawezekana zipo Taasisi za Serikal na banafsi zinasafirisha staff wao kwenye maeneo yao ya kazi kwa utaratibu maalumu. Sambamba na hilo Kamati inashauri sana kuchukuliwa hatua kwa baadhi ya walimu wanaoishi kwenye maeneo ya karibu na skuli na hawafiki kazini kwa wakati na wengine wanatoroka.

3. PROGRAMU YA ELIMU YA JUU

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatambua juhudi kubwa zinazofanywa na Wizara katika kuendeleza masomo ya elimu ya juu kwa vijana wetu. Kazi kubwa imefanywa na Serikali katika kuongeza mikopo kwa vijana wetu katika mwaka wa fedha unaomalizika 2017/18. Katika bajeti ya mwaka huu unaomalizika programu hii ilitengewa shilingi bilioni 23.4 ambapo Kwa mwaka huu wa fedha fedha hizo zimeongezwa kufikia shilingi bilioni 26.9.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuwakopesha fedha vijana wetu ambapo idadi ya

wanafunzi waliofaidika ni 2,721 na kiasi cha shilingi bilioni 10.13 kilipatikana ikiwa sawa na asilimia 99.3 cha Makadirio. Hata hivyo, Bado kuna kikwazo cha mikopo kwa wafanyakazi wa Serikali ambao hawaruhusiwi kukopa ingawa wanakopesheka. Kamati yangu inashauri Serikali kufikiria upya agizo hilo kwa kuruhusu baadhi ya wafanyakazi wa fani adimu ambazo wafanyakazi wanataka kujiendeleza wapatiwe mikopo, kama vile fani za afya, uhandisi wa vifaa tiba na walimu wa ufundi n.k.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kimeendelea na kazi zake za kutoa mafunzo ya fani mbali mbaali katika ngazi ya shahada za juu. Kamati yangu naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kungiza fedha za ruzuku SUZA ili kusaidia kazi za maendeleo zilizongezeka kutokana na Chuo hicho kuunganishwa na vyuo vyengine vya Serikali. Kamati yangu inaomba Serikali kwenye bajeti zinazofuata kuongezwa ruzuku hiyo ili kuharakisha kazi za maendeleo za SUZA.

Mheshimiwa Spika, kamati yangu bado inakumbusha utatuzi wa changamoto ya uvamizi ya maeneo ya SUZA katika Kampasi zake mbali mbali, wapo wananchi wamevamia maeneo ya Kampasi ya Chuo Kikuu na kufanya sehemu za Makaazi na biashara. Kamati inashauri hatua za haraka zichukuliwe kuyahami maeneo ya chuo kikuu ili yasiendelee kuvamiwa. Vile vile tunaomba sana Serikali iharakishe kuyapima na kutoa hati miliki za umiliki wa maeneo ya ardhi ya SUZA ili kuepusha watu wasiokuwa na nia njema kuvamia maeneo hayo.

4. PROGRAMU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

Mheshimiwa Spika, programu hii inashughulika na mafunzo ya elimu mbadala na watu wazima, mafanikio makubwa yamepatikana kwa kuviimarisha miundombinu ya kusomea. Kwa mwaka wa fedha unaomalizika wa 2017/18 programu hii imetengewa jumla ya shilingi bilioni 17.1 na kwa mwaka huu wa fedha 2018/19 zimetengwa shilingi bilioni 24.5, ambao ongezeko hili tunategemea litasaidia kutatuwa changamoto ambazo tunazionesha.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, Kamati yangu bado haijaridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa Chuo cha Amali cha Daya Mtambwe na kile cha Makunduchi ambavyo ujenzi wake unaenda taratibu mno. Vyuo hivyo vipo katika hatua ya ujenzi muda mrefu, tunashauri sana katika mwaka huu wa bajeti jitihada zifanyike kuhakikisha maendeleo ya ujenzi wa vyuo hivyo yanapiga hatua za kuridhisha ili vijana wetu wapate maeneo mazuri ya kujifunza kazi za amali.

Mheshimiwa Spika, kamati yangu inatambua juhudi kubwa zinazofanywa na walimu wa vyuo vya amali na watu wazima, hata hivyo, tunaomba sana Serikali iwatazame walimu wa Vyuo vya Amali na watu wazima ambao wanafundisha fani za ufundi ambazo zinajumuisha vitendo zaidi kuliko nadharia. Ni vyema maslahi yao yakaimarishwa kwa kupatiwa posho maalumu la kazi ngumu hasa ukizingatia vijana wanaosomeshwa hapo wanatoka wakiwa weledi wa fani mbali mbali ambazo wanaweza kujiajiri wenyewe.

5. PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU

Mheshimiwa spika, Kwa mwaka wa fedha unaomalizika program hii ilitengewa shilingi bilioni 6.07 na kwa mwaka huu wa fedha zimetengwa kiasi cha shilingi bilioni 7.7, Kamati yangu inatambua shughuli nyingi zinazohusika katika programu hii na inaomba sana Serikali na Wizara kuhakikisha programu hii inapata fedha za kutosha ili shughuli hizo zifanyike kwa ufanisi. Sekta kadha muhimu katika kuimarisha ubora wa elimu zinahusika katika programu hii kama vile Taasisi ya Elimu Zanzibar, Baraza la Mitihani, Mrajis wa Elimu, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Shirika la Huduma za Maktaba, elimu mjumuisho, Vituo vya Mafunzo ya Walimu, TEHAMA na michezo. Kamati bado ina wasi wasi kama fedha zinazotengwa katika programu hii zinakidhi kuleta matokeo yanayotarajiwa katika utekelezajiwa programu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaipongeza Taasisi ya Elimu Zanzibar ambayo imeanzishwa chini ya sheria namba 4/2016 kwa kazi nzuri ya kutayarisha mitaala ya elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi za maandalizi, msingi, sekondari na mafunzo ya ualimu.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kazi hiyo Kamati inashauri Taasisi ya Elimu kuzingatia upya na kupitia mitaala ya ngazi ya msingi hasa kwa madarasa ya awali ya msingi ambapo Kamati imepata malalamiko kuwa wanafunzi wakiwa na umri mdogo

wanasomeshwa masomo manane ambayo ni mengi sana kwa watoto wa umri wa miaka sita.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa nyenzo za kufundishia katika ngazi ya maandalizi ni muhimu na Kamati inashauri sana kupitia bajeti ya mwaka huu kuongeza fedha kwa ajili ya kuwawezesha walimu kutengeneza nyenzo na vifaa hivyo kwa njia rahisi.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani la Zanzibar linafanyakazi kubwa ya kutayarisha mitihani na kuwapima wanafunzi wetu masomo yao. Tunaipongeza Serikali kwa kuhakikisha fedha zinapatikana za kufanyia shughuli za matayarisho na uchapaji wa mitihani. Aidha tunalipongeza sana Baraza la Mitihani kwa kuongeza kiwango cha usiri wa mitihani na kuzuiwia kuvuja hii imetokana na hatua za Baraza la Mitihani kuongeza mikakati mbali mbali ya utendaji ikiwemo kuchapisha mitihani hiyo kupitia kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatambua kazi kubwa inayofanywa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Kamati inashauri mwaka huu wa fedha kuongezwa wigo wa ukaguzi kwa skuli binafsi ambazo zinafanyakazi ya kusaidiana na juhudi za Serikali kundeleza elimu nchini. Tunashauri ukaguzi huo ufanyike ili kuhakikisha kuwa Skuli hizo zinaendesha shughuli zake kwa mujibu wa Sheria, taratibu na miongozo ya Wizara ya Elimu na ubora wa elimu uzingatiwe kwanza kuliko kujali mapato ya fedha kwa skuli.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Maktaba ni muhimu kwa kuwaongezea uwezo wanafaunzi wetu na utamaduni wa kujisomea na kujiongezea maarifa. Shirika la Huduma za Maktaba linafanya vizuri katika kuhakikisha wigo wa wananchi wetu kujiongezea maarifa unafikiwa kupitia huduma za Maktaba. Kamati inashauri kuipatia nyenzo za usafiri na kompyuta ili iweze kufanya majukumu yake vizuri. Shirika hili linahitaji kufanyiwa mapitio ya muundo wake kwa vile Kamati imepata maoni kuwa muundo wake wa kuwa Shirika unalifanya lionekane kama chombo cha kutengeneza faida badala ya kutoa huduma.

6. PROPGRAMU YA UTAWALA NA UONGOZI

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudi za Wizara za kuajiri walimu wapya katika fani mbali mbali hasa za walimu wa masomo ya sayansi ambao ni wachache na mahitaji kuwa makubwa. Tunaomba zoezi hili liendelee katika kila mwaka wa bajeti ili kupunguza uhaba wa walimu unaokabili Skuli zetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo Kamati yangu inatambuwa bado tatizo la uhabawa walimu, wakutubi na Wasaidizi wa maabara lipo kubwa katika skuli zetu Unguja na Pemba. Kamati yangu imeshauri katika ripoti zake mbali mbali kuwa wakati umefika kwa changamoto za kiutumishi za walimu zitatuliwe kwa Serikali kuunda chombo maalumu katika mfumo wa Tume ya Utumishi ya Walimu kama ilivyo kwa nchi nyingi duniani ikiwemo jirani zetu Tanzania bara.

Mheshimiwa Spika, mbali na ushauri huo wa Kamati hii, Walimu wenyewe kupitia chama cha Walimu Zanzibar (ZATU) wametowa wazo la kuundwa kwa Tume ya Utumishi ya Walimu mbele ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein, na Mheshimiwa Rais pamoja na kuona kuwa jambo hilo ni mapema ametoa rai kama kuna haja ya walimu kuwa na tume ya utumishi basi zitumike njia za kuwasilisha hoja hiyo Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona kuwa wazo hilo linaweza kutafutiwa njia ya kuletwa Serikalini na Kamati yangu inashauri njia hizo zitafutwe ili Tume ya Utumishi ya Walimu iundwe na kutatuwa changamoto nyingi za kiutumishi zinazowakabili walimu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa Walimu kupitia chama chao kutofanyika kwa vikao vya pamoja na Wizara vya kujadili na kutatuwa changamoto zinazowakabili walimu. Sote tunakumbuka mnamo mwezi Februari, 2018 Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Chama cha Walimu Zanzibar ameagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wakae pamoja na Chama cha Walimu katika vikao rasmi ambavyo ni mara mbili kwa mwaka ili kutatuwa changamoto zinazowahusu walimu. Kamati yangu inazo taarifa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haijatekeleza agizo hilo mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inachukuwa nafasi hii kuitaka Wizara kutekeleza agizo hilo la Rais kwa kupanga vikao hivyo rasmi na Kamati inawaahidi walimu kuwa itaendelea kusimamia kuhakikisha kuwa agizo hilo la Mheshimiwa Rais linatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya sera ya elimu ni muhimu na Kamati yangu inasisitiza kuwa kwa mwaka huu wa fedha sera hiyo ya elimu ya mwaka 2006 ifanyiwe mapitio na kurekebishwa katika maeneo mbali mbali ambayo yanaonekana kuleta changamoto. Kamati yangu bado ina mashaka na mfumo wa ufaulu wa wanafunzi kuvukishwa darasa kutoka msingi kwenda sekondari wakiwa hawana matayarisho ya kukabiliana na mitihani ya kitaifa katika ngazi ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kwamba kuna mwanafunzi wa Sekondari hawajuwi kusoma wala kuandika, tunajiuliza mwanafunzi huyo anafikaje ngazi ya Sekondari akiwa hajuwi kusoma wala kuandika. Kamati yangu inaomba sana mfumo huu tunaokwenda nao wa kuwavukisha wanafunzi kutoka madarasa ya msingi moja kwa moja mpaka Sekondari upitiwe upya kwani ndiyo mfumo ambao unatusababishia ufaulu mbovu katika mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne. Tunaomba hatua za haraka zichukuliwe kuhakikisha kuwa mwanafunzi havukishwi darasa la msingi kwenda sekondari ikiwa hajuwi kusoma wala kuandika.

Mheshimiwa Spika, katika programu hii ya utawala na uongozi pia kuna usimamizi wa masuala ya ujenzi Kamati yangu imebaini

kuwa hii si sahihi. Inafaa Wizara iunde programu maalumu kusimamia mambo yote ya ujenzi na matunzo ya skuli, vyuo na vyuo vikuu. Pia kamati inashauri sana mikataba ya ujenzi kwa washauri elekezi na wakandarasi itazamwe kwa undani. Kamati imegunduwa kwua wakandarasi wengi wa majengo ya Wizara hawafanyi vizuri, wanaripua tu kazi zao.

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kipindi chote kuonesha mashirikiano makubwa na kamati yetu, tumekaa nao katika kupitia fungu hili la K01 na mambo mbali mbali tumeshauriana na hatua za kuchukuwa. Tunasisitiza kuwa Kamati yangu itaendeleza mashirikiano hayo kwa kufuatilia utekelezaji wa ahadi zote zilizoahidiwa na Wizara hasa suala la malipo ya malimbikizo ya stahiki mbali mbali za walimu.

Mhehishimiwa Spika, nawaomba sana walimu wote wa Unguja na Pemba waendelee kuchapa kazi na Kamati hii itahakikisha kuwa madeni yao na maslahi yao mengine yanalipwa kwa vile kuna ahadi kutoka kwa Wizara kuwa yatafanyikwa kazi haraka katika bajeti ya mwaka huu. Tunaiagiza tena Wizara kufanya vikao vya kawaida vya majadiliano na Chama cha Walimu Zanzibar. Ni imani yetu kwamba vikao hivi vitaleta taja kati ya uongozi wa Wizara na Walimu ambao ndio wenye chama hiki.

Mheshimiwa Spika, Chama hiki kina wajibu wa kusimamia uwajibikaji wa walimu, kutetea maslahi na hadhi ya walimu. Kamati haioni mantiki walimu wenye sifa ambao wanajitolea katika maskuli ndak ya maneo yao kuachwa kwenye ajira na kuajiriwa walimu wanaoishi mbali ya skuli. Kamati imepata habari kwamba kuna walimu wengi hawajathibitishwa kazini, kinyume na utaratibu. Kwanini?

Mheshimiwa Spika, vile vile tunaomba Wizara kuyapeleka mapendekezo ya bajeti yake katika Kamati ya Uongozi ya Wizara kwa kujadiliwa na kupata Baraka za wajumbe waote na kamati ya Uongozi kama taratibu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Naomba nichukuwe fursa hii tena kwa dhati kabisa kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye tumeona nguvu, juhudi na kazi kubwa anayofanya kuinuwa sekta ya elimu na mara hii ameongeza bajeti ya Wizara ya elimu kwa ongezeko la asilimia 19% tunampongeza sana kwa kusikia kilio cha Kamati cha kuhakikisha kila mwaka bajeti ya Wizara ya Elimu inaongezwa kadiri uwezo wa Serikali unavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Nachukuwa fursa hii tena kuwapongeza walimu wote wa Unguja na Pemba kwa kazi ngumu wanayofanya ya kuwasomesha vijana wetu, wito wetu kwao, kujitahidi kufanyakazi

kwa uweledi na maadili, haki zao na stahiki tutahakikisha tunaisimamia Wizara kuzilipa.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuwaomba wajumbe wa Baraza hili kujadili bajeti hii na hatimaye kuipitisha ili Wizara iende kutekeleza majukumu ya kusomesha vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wajumbe wako kwa kunikiliza na nakushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha maoni haya kwa niaba ya Mwenyekiti.

Ahsante, na naunga mkono hoja.

.....

Mheshimiwa Tatu Mohammed Ussi,

M/Mwenyekiti,

Kamati ya Ustawi wa Jamii,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar